# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

**Mtaa wa Nkoani,**
**S.L.P 273,**
**55103 RUKWA,**
**Barua pepe: rbcrukwa@pccb.go.tz.**
**TANZANIA.**

**Tovuti: www.pccb.go.tz**

**Tarehe 24/07/2020**

# TAARIFA KWA UMMA

## TAARIFA YA UTENDAJI KAZI MWEZI APRILI HADI JUNI, 2020 -TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA MKOA WA RUKWA

Ndugu waandishi wa habari, tunapenda kuwajulisha wananchi wa mkoa wa Rukwa kwamba, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Rukwa imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kazi kwa kushirikiana na ofisi zake zote za wilaya na wananchi kwa ujumla, ambapo kwa robo ya nne ya mwaka mwezi Aprili hadi Juni, 2020 imetekeleza mambo yafuatayo katika eneo la uchunguzi na mashtaka, ukaguzi wa miradi ya maendeleo na uelimishaji umma.

### 1. Uchunguzi na Mashtaka

Katika kipindi hiki tulipokea jumla ya taarifa 34 ambapo kati ya hizo, taarifa 12 zilitoka Halmashauri ya Manispaa, taarifa 8 zilitoka Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, taarifa 09 zilitoka Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo na taarifa 05 zilitoka Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi. Taarifa zote hizi zipo katika hatua mbalimbali za kiuchunguzi.

Aidha katika kipindi hiki tulifungua kesi nne (4). Mahakamani ambazo ni:

1.1. Kesi CC. No. 82/2020 imefunguliwa tarehe 18/06/2020 katika mahakama ya wilaya ya Nkasi, kesi hii inamhusu ndugu Jovin Victor Kahambo Afisa Uhamiahi wilaya ya Nkasi, kuomba rushwa ya tshs. 150,000/= na kupokea tshs. 100,000/= kutoka kwa watu watatu aliyewatuhumu kuwa ni wahamiaji haramu ili asiwachukulie hatua za kisheria.

1.2. Kesi CC. No 07/2020 imefunguliwa tarehe 21/06/2020 katika mahakama ya wilaya ya Sumbawanga mjini, kesi hii inamhusu ndugu Andondile Mwakitalima aliyekuwa Mkufunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii cha Paradize Sumbawanga mjini kuomba na kupokea rushwa ya ngono kutoka kwa Mwanachuo ambaye alimuahidi kumpa upendeleo wa alama ambazo zingemwezesha kufauli katika masomo yake.

1.3. Kesi CC. No. 66/2020 imefunguliwa tarehe 24/06/2020 katika mahakama ya wilaya ya Kalambo, kesi hii inamhusu Tabibu Msaidizi (*Clinical Officer*) wa kituo cha Afya cha Matai Wilayani Kalambo ndugu Eliud Joshua Humbo ambaye aliomba na kupokea rushwa ya Tshs. 100,000/= kutoka kwa mgonjwa aliyekuwa na rufaa ya kwenda Hospitali ya Rufaa ya Mkoa mjini Sumbawanga na kuimfanyia upasuaji wa tumbo (Henia) bila kufuata taratibu.

1.4. Kesi CC No. 159/2020 imefunguliwa tarehe 30/06/2020mahakama ya Wilaya ya Nkasi, kesi hii inamhusu ndugu Ezekiel Joseph Nzuki, Afisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Wilaya ya Sumbawanga mjini kuomba na kupokea rushwa ya tshs. 500,000/= kutoka kwa mfanyabiashara mmoja wa Sumbawanga mjini ili amsaidie kupunguza kadirio la kodi ambalo alimwongezea katikati ya mwaka.

2. **Ukaguzi wa miradi ya maendeleo, udhibiti wa mapaato ya serikali na uokoaji wa fedha za wanachama wa SACCOS mbalimbali.**

Ndugu waandishi wa habari, pamoja na takwimu hizo hapo juu, naomba nitoe ufafanuzi kuhusu tuhuma za rushwa na utapeli unaofanywa na viongozi wa SACCOS mbalimbali, ukusanyaji mapato ya Halmashauri za wilaya kwa njia ya POS pamoja udhibiti wa mapato ya serikali katika miradi ya maendeleo.

Kipindi cha kuanzia mwezi Aprili hadi Juni, 2020 ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Rukwa imefanikiwa kuokoa kiasi cha fedha tshs. 169,828,000/= zilizokuwa zimefujwa na viongozi wa SACCOS mbalimbali, miradi ya maendeleo pamoja na wakusanyaji sugu (*defaulters*) wa mapato serikali kwa njia ya POS katika Halmashauri za wilaya, fedha hizi tulizirejesha kwa wahusika tarehe 11/06/2020 mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Rukwa ndugu Joakim Wangabo kama ifuatavyo:

**2.1. Udhibiti wa mapato ya serikali katika miradi ya maendeleo**

Ndugu waandishi wa habari, moja ya majukumu ya Takukuru ni kukagua miradi ya maendeleo na katika kutekeleza jukumu hili kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni, tumenya kurejesha tshs. 45,315,000/= baada ya kufanya ukaguzi katika Mradi wa Umwagiliaji wa Katongolo kule wilayani Nkasi baada ya kufanya ukaguzi huo na kubaini kuwa Mkandarasi ambaye ni Kampuni ya Girson Investments Ltd alikuwa amelipwa fedha nyingi kuliko kazi alizokuwa ametekeleza. Kipaumbele kwa serikali ni kuhakikisha kuwa fedha hii inarejeshwa Serikalini wakati hatua nyingine za kisheria zikiendelea. Mpaka sasa Mkandarasi amekwisharejesha Tshs. 45,000,000/= ambazo zilirejeshwa kupitia Akaunti maalum ya Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU iliyoko Benki Kuu ya Tanzania (BoT). Aidha, tshs. 315,000/= ni fedha ambazo zilirejeshwa na Afisa Uhamiaji wilaya ya Nkasi

baada ya TAKUKURU kubaini kuwa Mtumishi huyo alipokea kiasi hicho cha fedha kutoka kwa Wahamiaji wa nchi jirani ambao walikuwa wanasafiri kwa basi kupitia nchini mwetu kwenda nchi

za kusini mwa Afrika wakiwa na vibali vyote na kueleza kuwa alipokea kama zawadi, pamoja na kuchukuliwa hatua za kinidhamu pia alitakiwa kurejesha fedha hii ambayo pia iliingizwa katika akaunti maalum ya Benki Kuu.

### 2.2. Fedha zilizookolewa kutoka SACCOS mbalimbali tshs. 96,456,250/=

Ndugu waandishi wa habari kati ya fedha hizo kiasi cha tshs. 56,700,000/= ni fedha waliyorejeshewa Walimu Wastaafu 39 wa SACCOS ya CHAUWAMI ambayo inahusisha walimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo. CHAUWAMIi iliundwa kabla ya wilaya ya kalambo haijaanzishwa.Walimu hawa walikuja Takukuru na kulalamika kuwa tangu walipostaafu viongozi wa chama hiki hawajawalipa Amana zao na hawana dalili za kuwalipa na wamefuatilia kwa vipindi vya miaka mmoja hadi minne.

Katika uchunguzi tulioufanya tulibaini kuwa uongozi wa SACCOS hiyo walitumia AKIBA na HISA za Wanachama wake zote kinyume na Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013. Fedha hizi tuliwabana na wamezirejesha zote.

Ndugu waandishi wa habari fedha tshs. 39,756,250/= tuliwakabidhi viongozi wa Nkasi Teachers SACCOS ambazo uongozi wa awali wa SACCOS hiyo uliandaa nyaraka na kuwakopesha watu wasio wanachama kinyume na Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba 6 ya mwaka 2013.

Uchunguzi huu ulitokana na taarifa ya COASCO ambayo waziri wa Kilimo alimkabidhi Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU kwa ajili ya kuifanyia kazi. Fedha hizi zilingizwa katika akaunti ya Chama l

Ndugu waandishi wa habari tshs. 1,345,000/= zilikuwa fedha za SACCOS ya MAKUPA iliyopo Wilayani Nkasi ambazo ni fedha zilizokopeshwa kwa wanachama lakini wakagoma kuzirejesha kwenye SACCOS yao kwa mujibu wa masharti ya muda wa kufanya Marejesho ya Mikopo yao, na hizi pia tulizikabidhi kwa viongozi wa Saccos hii.

### 2.3. Fedha tshs. 34,212,000/= zilizookolewa toka kwa wadaiwa sugu (defaulters) wa ukusanyaji mapato kwa njia ya POS Halmashauri ya wilaya ya Sumbawanga:

Ndugu waandishi wa habari atika kipindi cha mwezi Aprili hadi Juni, 2020 tumeshiriki katika kuisaidia Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga kukusanya fedha ambazo ama zilikuwa zimepotea au zilikuwa hazijawasilishwa na kuingizwa katika mfumo na katika Akaunti za Halmashauri kama taratibu za fedha za Serikali za Mitaa zinavyoelekeza. Mwaka 2019 Mkuu wa Mkoa wa Rukwa

alituagiza na tulifanikiwa kukusanya zaidi ya Tshs 325,000,000/=. Tarehe 08.06.2020 tuilipokea taarifa ya “Defaulters” kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga baada ya yeye kuagizwa na kikao cha Baraza la Madiwani cha tarehe 06.06.2020 kuiomba TAKUKURU iwasaidie kukusanya madeni sugu kutoka kwa baadhi ya watendeji wa Kata na Vijiji katika Halmashauri hiyo. Kwa kipindi cha siku mbili TAKUKURU Mkoa wa Rukwa ilifanikiwa kukusanya jumla ya Tshs. 34,212,000/= ambazo tulimwomba Mkuu wa Mkoa kuzikabidhi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Sumbawanga na zoezi la ukusanyaji linaendelea .

3. **Elimu Kwa Umma**

Ndugu waandishi wa habari, ni wajibu wetu kushirikisha umma katika juhudi za kuzuia na kupambana na rushwa kupitia mikutano ya hadhara, semina, vipindi vya redio pamoja na maonesho, ambapo watu wa kada na rika mbalimbali katika kipindi hiki wameelimishwa hasa katika maeneo ya kukataa na kutoa taarifa dhidi ya vitendo vya rushwa ya ngono na elimu ya madhara ya rushwa katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020. Vilivile tumewaelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa kukataa na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kupitia Kampeni ya UTATU, matumizi ya TAKUKURU APP na Vunja Ukimya Kataa Rushwa ya Ngono.

Katika kipindi hiki tumefanikiwa kuimarisha klabu 24 za wapinga rushwa katika shule za msingi na sekondari baada ya shule kufunguliwa tarehe 29/06/2020. Aidha kupitia semina 7 na mikutano ya hadhara tumefanikiwa kuwaelimisha wananchi kuhsu umuhimu wa kushiriki kudhibiti vitendo vya rushwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. .

Uelimishaji uliofanyika umechangia kupokelewa kwa taarifa nyingi za vitendo vya rushwa na makosa yahusianayo na rushwa, ni vyema kwamba viongozi na watumishi wa maeneo yanayoonekana kuongoza kwa kulalamikiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa wachukue hatua stahiki ikiwa ni pamoja na kuimarisha mikakati yao ya ndani ya kudhibiti rushwa.

Ndugu waandishi wa habari, katika robo ya kwanza ya mwaka mwezi Julai hadi Septemba, 2020 TAKUKURU Mkoa wa Rukwa itaendelea kuwahamasisha wananchi kushiriki kivitendo katika kuzuia rushwa na tutaendelea kutoa elimu ya rushwa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge pamoja na Madiwani. Aidha tutaendelea kufuatilia madeni ya vyama vya ushirika, wadaiwa sugu wa mapato ya Halmashauri za Wilaya pamoja na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha kwamba miradi inayotekelezwa na wakandarasi inalingana na thamani halisi ya fedha iliyotolewa na serikali (*value for money*).

**Wito:**
Ndugu Wanahabari, tukumbuke kwamba mwaka huu wa 2020 ni mwaka wa uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani, TAKUKURU tunaendelea kupokea taarifa za vitendo vya rushwa ambavyo vinafanywa na baadhi ya wananachama wanaowania nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi ujao, ni vema wananchi hawa wanaonyemelea majimbo na kata mbalimbali wakaheshimu sheria, kanuni na taratibu za uchaguzi.

TAKUKURU inawataka wanasiasa wote wanaomba uongozi mbalimbali ndani ya vyama kutoa ushirikiano wa dhati TAKUKURU inapohughulikia rushwa kwenye uchaguzi, pia wajiepushe na rushwa na yale yanayokatazwa na sheria za uchaguzi kwani mwisho wa siku vitendo hivi vitawagharimu.

**HAMZA MWENDA**
**MKUU WA TAKUKURU (M) WA RUKWA**
**TAREHE: 17/07/2020**